

Ajenda ya NCD ya Ulimwenguni kwa

# **AJILI YA UNYUMBUKAJI NA UFUFUZI DHIDI YA COVID-19**

---

**3 MNARA WA :**  
**12 MAPENDEKEZO**



# YALIYOMO

## MUHTASARI MKUU:

Ajenda ya ulimwenguni katika kuitikia mgogoro wa leo, jitayarishie tishio za kesho **3**

## MUKTADHA WA SERA:

Janga kuu la COVID-19 na magonjwa yanayoambukiza **4**

## MAPENDEKEZO:

Mazingatio badilishi, sera na matumizi ya umma ili kuimarisha unyumbukaji **6**

## MNARA WA 1

**Utawala:** Fafanua upya mazingatio na nguvu na kupima kile kinachofaa **7**

## MNARA WA 2

**Kinga:** Zingatia idadi ya watu kama njia ya kujitayarishia **15**

## MNARA WA 3

**Mifumo ya afya:** Mizuri zaidi na inayofaa kwa ajili ya siku za usoni **18**



Muhtasari mkuu:

# AJENDA YA ULIMWENGINI KATIKA KUITIKIA MGOGORO WA LEO, JITAYARISHIE TISHIO ZA KESHO

Muungano wa NCD umeunda Ajenda hii ya NCD Ulimwenguni kwa ajili ya Unyumbukaji na Ufufuzi dhidi ya COVID-19 kwa nia ya kuwafikia waundaji sera wanaotafuta kujiimarisha vizuri zaidi. Tunatambua kwamba janga liko mbali sana na kuisha na kwamba miitikio hadi sasa haijatosheleza, huku ikifichua kushindikana kwa uthabiti wa kimataifa na ikionyesha hali ya kutokuwa na usawa. Hata hivyo, mwitikio wa janga unatoa fursa ya kujifunza mafunzo na kuhakikisha kwamba uvumbuzi, rasilimali, na teknolojia zilizohamasishwa vyote vinayo athari badilishi ya kuangazia magonjwa yasiyoambukiza (NCDs) - magonjwa yaliyoenea na maarufu zaidi ulimwenguni ambayo kila mwaka yanawaua watu zaidi ya milion 40 na kusababisha idadi nyingine ya watu wapatao 100 kuingia katika ufukara.

Hatua na uwekezaji wa NCD havifai kuonekana tena kama jambo lililofikiriwa baadaye kuhusu magonjwa yaambukizayo na lililopuuzwa ndani ya huduma za afya, lakini kama kipengele muhimu cha unyumbukaji, ulinzi, usawa, na uthabiti wa kiuchumi. Haijalishi kama NCDs zinaangaziwa na hatua ya sera za siku za usoni, yakiwemo mazungumzo ya mkataba wa janga la kimataifa, itaimarisha au kuzorotesha ubora wa mwitikio wa janga.

Ajenda hii ya NCD ulimwenguni kwa ajili ya Unyumbukaji na Ufufuzi dhidi ya COVID-19 inaainisha suluhu za kufuzu pande zote ile kuhakikisha nchi zote zinaweza kufufuka kwa nguvu zaidi na kukumbatia siku za usoni zenye usalama zaidi na afya zaidi. Mapendekezo yamenuia kusaidia viongozi na watoaji uamuzi kumakinikia usawa, hatua ya sera yenye unafuu zaidi na uwekezaji ili kupatia nguvu afya ya idadi ya watu na kuimarisha mifumo ya afya yenye unyumbukaji zaidi. Hii inajumuisha watoaji uamuzi katika serikali za kitaifa, kotekote kwenye wizara na idara zote, uongozi wa huduma za umma ikiwemo mifumo ya afya, jopokazi la afya, taasisi za kimataifa, vyama vya uraia, taasisi za utafiti, filanthropia, na sekta ya kibinafsi vyote vikifanya kazi kwa nia ya kuboresha afya na maendeleo endelevu.

## **Mapendekezo 12 yaliyoainishwa katika ajenda hii yamewekwa katika makundi matatu ya minara:**

Ajenda hii inaongozwa na kanuni za usawa, ubora wa utunzaji, na kuwaweka watu mbele. Mapendekezo yanatokana na utaalamu kutoka kwa watalamu wa afya ulimwenguni, wakiwemo watu wanaoishi na NCDs na mashirika ya vyama vya kiraia.

---

**Kutabaruku:** Muungano wa NCD ungependa kushukuru wanachama wetu na Maoni Yetu, Kamati Shauri Ulimwenguni kuhusu Sauti Zetu kwa michango yao yenye thamani. Tunashukuru wanachama wa kundi la ushauri wa watalamu kwa mwongozo na usaidizi wao: Sir George Alleyne, Mkurugenzi Emeritus Pan-American Health Organisation, Barbados; Martin Bernhardt, Sanofi, Switzerland; Profesa Agnes Binagwaho, Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu, University of Global Health Equity, Rwanda; Richard Gregory, WHO, UHC2030, UK/Switzerland; Paula Johns, ACT+, Brazil; Fale Andrew Lesā, NCD Child, Samoa/New Zealand; Dkt. Andrew Schroeder, Direct Relief, Marekani; Dr Sudhvir Singh, Jopo Huru la Kujitayarishia na Mwitikio wa Janga, New Zealand/Norway. Aidha, shukrani zetu zinamwendea Ademola Osigbesan kutoka UNITAID kwa uhakiki wake.

Muktadha wa sera:

# JANGA KUU LA COVID-19 NA MAGONJWA YANAYOAMBUKIZA

COVID-19 imetikisa misingi ya mifumo ya afya na uchumi kote ulimwenguni na kugeuza uelewa wa kinachohitajika ili kuwa tayari kwa janga. Mwitikio katika nchi zilizofikiriwa kuwa zimejitayarisha kwa njia bora zaidi ulidhalilishwa na tishio liliopuuuzwa, ambalo halikutiliwa maanani awali katika viwango vya ulinzi wa afya: magonjwa yasiyoambukiza (NCDs). Watu wanaoishi na NCDs wamekuwa katika kitovu cha mgogoro huu kwenye mataifa yaliyo na mapato ya chini na vilevile ya juu. Kuwepo kwingi kwa NCDs kumesababisha ongezeko la vifo na magonjwa mionganoni mwa watu waliyo na COVID-19, kumeweka sehemu kubwa za idadi ya watu hatarini na kuyumbisha mifumo ya afya vilevile. Umekuwa ukweli mtupu kwamba serikali na taasisi za ulimwenguni zinakabiliana na janga kuu, pale ambapo janga hatari la COVID-19 linaendelea kufanya athari za janga kuu la NCDs kuwa kali zaidi.<sup>01</sup>

**“Huku tukiwa na mgogoro huu, lazima tutumie dirisha hili la fursa ili tusifanye kazi kwa upweke lakini kwa kushirikiana katika kuimarisha mfumo wa afya ya umma uliyofadhiliwa pale ambapo lazima tujitayarische kupigana na utofauti wa afya na kuunda jumuiya ambayo ina haki kwa kiasi fulani. Ufikivu wa kuwatunza watu wanaoishi na NCDs ni muhimu sana na lazima ufungamanishwe kwenye mifumo ya afya ili kukabiliana a mzigoto mara mbili wa magonjwa kwenye miaka iliyopita. Matatizo yanayotokana na janga yamebadilisha kwa kweli mifumo ya afya na kimsingi yanahusisha ushirikiano wa vyama vya kiraia na afya ya umma ili kufanya kazi pamoja na kujimarisha kwa njia bora zaidi.”**

**Shiriki katika Maoni Yetu, Sauti Zetu COVID-19 na Kuimarisha Ushauriano bora zaidi, India.**

Kabla ya janga, nchi zisizozidi 20 kote ulimwenguni ziliikuwa zikiendelea vyema katika hatua ya kupunguza vifo vya mapema vya NCD kwa theluthi moja kufikia 2030, kujitolea ambako serikali zilijitolea mnamo mwaka wa 2015 kama sehemu ya Shabaha za Maendeleo Endelevu (SDG3.4).<sup>02</sup> Kutochukua hatua kwa muda mrefu kwa serikali kwa NCDs kumezidisha gharama ya binadamu na uchumi kwa COVID-19. Kiwango kikubwa zaidi cha mamiloni ya watu mpaka leo amba walipoteza maisha yao au waliugua sana

kutokana na maambukizi ya COVID-19 walikuwa na hali tatanishi za afya zao mwilini mwao, sanasana ugonjwa wa presha, moyo, na kisukari. Uchunguzi unakadiria kwamba asilimia 60–90 ya vifo vya COVID-19 vimekuwa vya watu wanaoishi na NCDs moja au nyingine.<sup>03</sup> Juu kabisa ya hesabu za moja kwa moja kuhusu afya, Programu ya maendelelo ya Umoja wa Mataifa inakadiria kwamba janga linaweza kusukuma watu zaidi ya milioni 200 kwenye ufukara kufikia 2030.<sup>04</sup>


**Kategoria mbili za ugonjwa unatumika ndani ya idadi mahususi ya watu—maambukizi kutokana na virusi vya korona vinavyoathiri kupumua vizuri (SARS-CoV-2) na mseto wa magonjwa ya kuambukiza (NCDs). Hali hizi zinabanana ndani ya makundi ya kijamii kulingana na mifumo ya hali ya kutokuwa na usawa ambayo imekita mizizi katika vyama vyetu. Kujumuishwa kwa magonjwa haya kwa mtawanyiko wa utofauti wa kijamii na kiuchumi huku ukizungumzia athari kubwa za kila ugonjwa binafsi. COVID-19 si janga. Ni mfumo wa kuendeleza tu mawasiliano.”**

**Dkt. Richard Horton, The Lancet<sup>05</sup>**

Aidha, watu wanaoishi na NCDs wanapitia athari zisizowahusu moja kwa moja kwenye janga hili, kutokana na kutatizwa muhimu kwa huduma za afya, huku pia kukiwa na vipengele muhimu vya mifumo ya afya vikiwemo jopo la kazi vyote vimebadilishwa na vinaangazia COVID-19.<sup>06</sup> Idadi ingali inaongezeka kutokana na matibabu yaliyoahirishwa kwa ajili ya kiharusi, matatizo ya moyo au ugonjwa wa figo kucheleweshwa katika ugunduzi wa saratani, kushindikana kwa msururu wa nyenzo kwa ajili ya dawa za kuokoa maisha kama vile insulini, kuzuiliwa kwa makazi, utunzaji wa kupunguza maumivu na huduma za afya ya akili (ambayo yalitatzwa kwenye 93% ya nchi zinazoripoti kwa WHO) na huduma za afya za uneni. Lakini ni wazi kwamba athari ya jumla kuhusu afya ndani ya kila nchi itakuwa kubwa zaidi kuliko ile ya virusi vyenyewe.

Taasisi ya Hesabu za Afya na Utathmini (IHME) imekadiria kwamba, kufikia Mei 13 2021, kumekuwepo na vifo vya watu wapatao milioni 7.1 kutokana na janga hili.<sup>07</sup> Kiwango hiki ni zaidi ya maradufu ya kile kilichoripotiwa cha vifo milioni 3.3 kutokana na COVID-19. Tofauti inaelezewa kupidia kwa mambo

## Mchoro wa 1: Kuripotiwa ulimwenguni na vifo vya ziada vya COVID-19, 2020-2021, kufikia Mei 13 2021.



Chanzo: IHME Makadirio ya vifo vya ziada kutokana na COVID-19 | Taasisi ya Hesabu za Afya na Utathmini ([healthdata.org](http://healthdata.org))<sup>i</sup>

mbalimbali, yakiwemo vifo vya mapema kutokana na utunzaji wa afya uliochelewa au ulioahirishwa, na kuongezeka kwa matumizi ya pombe na dawa za kulevyta, sawasawa na uwezekano wa kutoripoti sahihi.

Hali ya kutokuwa na usawa ndani na kati ya nchi vyote vinaonyeshwa kwenye mzigo wa NCDs na hali hizi zinaangaziwa zaidi kuititia kwa kiwango tofauti cha COVID-19 miiongoni mwa makundi tofauti ya idadi za watu. NCDs na COVID-19 vyote vinaathiri watu kwa njia tofauti, watu ambaao wamepuuzwa na kubaguliwa, kutokana na unyonyaji, hali ya ajira, umri, mbari au kabila.<sup>08</sup> COVID-19 imefichua vibaya sana hali ya kutokuwepo na usawa iliyokita mizizi na dhuluma iliyopo ndani ya jumuiya zote. Watu walio katika jumuiya zilizodhulumiwa wapo pia kwenye mistari ya mbele ya athari ya kiuchumi na wanakumbwa na machaguo magumu zaidi kutokana na vizuizi vya kutembea, kufanya kazi na utangamano wa kijamii. Hali hizi za

kutokuwa na usawa zinaendelea kuongezeka wakati serikali na jumuiya ya kimataifa zinashindwa kutekeleza mwitikio wa COVID-19 wenye usawa, bila ya kutilia maanani ufikivu wa chanjo. Kujitolea kwa kimataifa ili kupitia kipao mbele wale wanyonge zaidi na kutoacha yeote nyuma bado hakujaonyeshwa kwenye mwitikio.

**Si tu COVID-19 ambayo inawaua  
watu, ni kutopewa hadhi, ni ukosefu  
wa ufikivu, ni miaka ya kuishi ndani  
ya hali za afya ambazo hazijasimamiwa  
vyema kwa sababu ya rangi ya ngozi yako,  
au kabila lako, au kundi lako la kijamii."**

Dkt Mike Ryan, Shirika la Afya Ulimwenguni

<sup>i</sup> IHME: "Vifo vya ziada vinasababishwa na viendashaji sita vinavyoleta vifo ambavyo vinahusiana na janga na yale mamlaka ya uwekaji umbali yaliyoletwa na janga lenyewe. Viendashaji hivi siti ni: a) kima kile cha ziada cha vifo vya COVID-19, yaani, vifo vyote vinahusiana moja kwa moja na maambukizi ya COVID-19; b) ongezeko la vifo kutokana na utunzaji wa afya unaohitajika kucheleweshwa au kuahirishwa wakati wa janga; c) ongezeko la vifo kutokana na kuongezeka kwa matatizo ya afya ya kiakili yakiwemo msongo wa mawazo, ongezeko la matumizi ya pombe, ongezeko la matumizi ya afyuni au opioid; d) kupungua kwa vifo kwa sababu ya kupunguka kwa majeraha kwa sababu ya upungufu wa jumla katika magonjwa yanayohusiana na mamlaka ya uwekaji umbali; e) kupungua kwa vifo kutokana na kupungua kwa uenezaji wa virusi vingine, ambavyo sana ni mafua, virusi vya kupumilia kooni, na surua; na f) kupungua kwa vifo kutokana na baadhi ya mambo hatari, kama vile ugonjwa wa moyo na ugonjwa hatari wa kupumua, unaokuwepo wakati watu wanyonge ambaao wangekufa kutokana na hali hizi wanakuwa mapema zaidi kutokana na COVID-19. Ili kukadiria kwa usahihi vifo vya ziada vitokanavyo na COVID-19, tunahitaji kutilia maanani viendashaji hivi vyote sita vya mabadiliko katika vifo ambavyo vimefanyika tangu kuanza kwa janga."



Mapendekezo:

## MAZINGATIO BADILISHI, SERA NA MATUMIZI YA UMMA ILI KUIMARISHA UNYUMBUKAJI

Serikali na taasisi za kimataifa zina fursa ya kuchukua hatua kwa viendeshaji maarufu vya janga kuu la NCDs na COVID-19. Zaidi ya robo moja ya idadi ya watu wanaishi na NCDs moja au zaidi ambayo inawaweka katika hatari kubwa zaidi dhidi ya COVID-19.<sup>09</sup>

Hali hii haiwezi kupuuzwa tena kwa mwitikio na kujitayarishia kwa tishio za afya za siku za usoni. Kiini cha kufufuka kwa nguvu zaidi ni kuhifadhi idadi za watu katika afya bora zaidi, kwa kuhakikishwa kwamba NCDs zinapewa kinga zaidi, zinadhibitiwa na kutibiwa. Hali hii inahitaji kutatua mambo ya kimuundo

(kijamii na kiuchumi, kimazingira, kibashara, kisasa) yanayohusu COVID-19 na NCDs katika kila nchi na kotekote kwenye makundi yote ya umri. Hii inajumuisha ufukara na hali za kutokuwa na usawa, vizuizi vya kufikia utunzaji wa afya mzuri, na madhara yanayozuiliika yaliyosababishwa na tumbaku, pombe, vyakula na vinywaji vilivytengenezwa kisasa, na uchafuzi.

Ajenda hii inawasilisha mapendekezo ya sera 12 chini ya minara mitatu ya hatua badilishi: Utawala, Kinga, na Mifumo ya Afya.

# MNARA WA 1

## Utawala: Fafanua upya mazingatio na nguvu na kupima kile kinachofaa

Janga la COVID-19 limeonesha umuhimu wa miitikio ya serikali nzima. Hii inajumuisha Wakuu wa Serikali na wizara na idara zote kuweza kutekeleza mambo lingenishi ili kudhibiti virusi na kupunguza athari zake, kwa kadri inavyowezekana, katika sekta zote zikiwemo za afya, utunzaji wa kijamii, uchumi, ajira, elimu, na biashara. Kundi la kwanza la mapendekazo lililowasilishwa hapa hivyo basi linazingatia namna utoaji uamuzi na utawala vinaweza kuboreshwa.

**“**Ili kuhudumia jumuiya kwa njia yenyewe usawa zaidi na kuimarisha jumuiya zenyeye afya zaidi, unyumbukaji lazima uimarishwe kwenye jumuiya hizi na kulingana na mahitaji yao. Kunaweza kuwa na ukosefu wa unyumbukaji wa mifumo ya afya bila ya kuhusishwa kwa jumuiya kwenye viwango vyote.”

*Jopo Huru la Kujitayarishia Janga na Mwitikio<sup>10</sup>*

**“**Kama kuna funzo moja tulilojifunza kutokana na COVID-19, ni wajibu wa jumuiya na vyama vya kiraia katika kiwango cha kitaifa na ulimwenguni.”

**Mkurugenzi Mkuu Msaidizi wa WHO, kwa ajili ya Kujitayarishia kwa Dharura, Dkt Jaouad Mahjour, akiangazia Mkutano wa Afya Ulimwenguni wa74, Mei 2021.**



#1



## MAPENDEKEZO #1

## Jumuisha NCDs katika mwitikio wa COVID-19, ufulufuza, na mipango ya kujitayarisha

Mipango ya kitaifa ya mwitikio, ufulufuza, na kujitayarisha inafaa kuundwa kwa kutilia maanani mahitaji yanayowabana zaidi katika jumuiya.

Katika suluhisho la Mkutano Mkuu wa UN 2020 kuhusu COVID-19, serikali zilijitolea zaidi "kupatia nguvu zaidi jitihada za kuangazia NCDs kama sehemu ya Uwepo wa Afya Ulimwenguni (UHC) kutambua kwamba watu wanaoishi na NCDs na wale walio na mtagusano wa mambo makuu ya hatari wako katika hatari kubwa zaidi ya kuwa na dalili kali za COVID-19 na ni mionganini mwa wale walioathirika zaidi na janga".<sup>11</sup> Hadi sasa hata hivyo, nchi 16 ndizo zimeripoti kwamba usimamizi wa NCD katika huduma muhimu unajumuishwa katika mwitikio na mipango ya ufulufuza wa kitaifa wa COVID-19.

Kuitikia mahitaji ya dharura ya afya ya jumuiya kunahitaji kuendelea na kuchukua fursa ya kuboresha NCD na huduma za afya ya akili - vikiwemo kinga, uchunguzi, ugunduzi, matibabu, marekebisho na utunzaji wa maumivu - kama swala la dharura, ili kupunguza kuteseka zaidi kunakoweza kuzuilia. Kukatizwa kwa kiasi kikubwa kwa utunzaji wa NCD, kukiwemo uchunguzi na ugunduzi, kunaendelea kuongeza pakubwa vifo kwenye janga hili. Kukatizwa huku kunaunda idadi kubwa ya watu wanaosubiria kupata utunzaji, kotekote kwenye NCDs zote na hali za afya ya kiakili.

Utiliaji maanani maalum unahitajika kwa makundi yaliyotengwa na idadi ya watu waliodhulumiwa zaidi, pale ambapo maswala ya hatari kwa magonjwa ya kuambukiza na NCDs yamefungamanishwa. Hali hii inajumuisha watu milion 68 ulimwenguni ambao kwa sasa wanaishi katika mazingira ya kusaidiwa, wamehamishwa na migogoro na majanga ya kimaumbile, kama vile jumuiya kuathirika pakubwa na mabadiliko ya hali ya hewa. Hii imefuatwa na ongezeko la utashi wa utunzaji wa NCD na huduma za afya ya akili na bado imeonekana kuendelea kuongezeka. Mahitaji ya watu wanaoishi na NCDs katika mazingira haya yanahitaji usaidizi wa kimataifa kwa ajili ya mwitikio ulioboreshwaa katika utunzaji wa afya kuu ndani ya

mifumo ya afya ya kitaifa, ukiwemo ufikivu kwa wafanyakazi wa afya wa jumuiya, ugunduzi, matibabu na dawa za NCDs kali zaidi, pamoja na hali salama za kuishi, vyakula vyenye lishe bora na usafi mzuri.

### Mifano ya kuhemsha:

**Bahrain** inatambulika kwa hatua ya kuunganisha NCDs kwenye mipango ya ufulufuza wa kitaifa, kutohaka na uhushishwaji wa Mkurugenzi wa NCDs katika Wizara ya Afya ndani ya kamati yao ya kitaifa ya mwitikio wa COVID-19.

Nchini **Ghana**, Rais alitumia hotuba kadhaa za kitaifa zilizorushwa hewani kwenye televisheni kuangazia COVID-19 ili kuhamasisha NCDs na mambo makuu yanayosababisha hatari husika.



© Shutterstock

#2



### Kiungo (cha kufuata) cha Mikakati ya Ulimwenguni Kuhusu Uhusishwaji wa Watu Wanaoishi na NCDs: Kijisanduku cha maandishi:



Mikakati ya Ulimwenguni kuhusu Uhusishwaji wa Watu Wanaoishi na NCDs inatoa kanuni muhimu na mikakati maarufu ya kuwaweka watu wanaoishi na NCDs na jumuiya katika kitovu cha mwitikio wa NCD. Watoaji huduma wanahimizwa kupidisha Mikakati ya Ulimwenguni, inayotambua kwamba sauti za watu wanaoishi na NCDs, na jumuiya na chama cha kiraia chenye uthabiti ni lazima katika kutimiza shabaha za afya na maendeleo - katika viwango vya ulimwengu, kimaeneo, kitaifa, na mashinani.

#### MAPENDEKEZO #2

## Husisha jumuiya katika utoaji uamuzi

Ili kuelewa mahitaji ya watu, uhusishwaji wa jumuiya, lazima ufungamanishwe katika mwitikio wa kitaifa na mipango ya ufufusi na maendeleo na matokeo ya mkataba wa janga, huku watoaji uamuzi wakihitaji kujumuisha wale walio katika hatari kubwa zaidi.<sup>12</sup>

Hii inajumuisha watu wanaoishi na hali hatari zikiwemo NCDs, ulemavu, VVU, kifua kikuu na 'kuugua COVID kwa muda mrefu'. Watoaji uamuzi lazima pia kwa nadharia wafikie makundi ambayo mara nyingi huachwa nyuma: Watu wazee zaidi, wa mbari mbalimbali, na makabila madogomadogo, jumuiya za kiasili, watu wanaoishi katika nyumba za vibanda mijini, jumuiya za vijijini au mbali na miji, mataifa yanayoendelea kwenye visiwa vidogo, na LGBTQ+ na makundi mengine yaliyotengwa. Wanawake wanaathirika pakubwa zaidi kutoptana na hali ya kiuchumi kwenye janga na mamilioni ya watoto na vijana wanaishi na NCDs (kwa mfano, zaidi ya watoto na vijana milioni 4.5 wanaishi na kisukari<sup>13</sup>). Lazima wapewe pia zingatio maalum katika uhusishwaji wa jumuiya.

Jopo Huru la Kujitayarishia na Kuitikia Janga liligundua kwamba miitikio ya kitaifa dhidi ya COVID-19 yenye ufanisi zaidi ni ile ambayo ilihuushwa jumuiya za ndani ili kuimrisha mifumo ya afya inayonyumbuka, na kufahamisha utoaji huduma, utoaji uamuzi na utawala ili kutimiza mahitaji ya jumuiya.<sup>14</sup> Serikali zilijitolea katika Mkutano wa Kiwango cha Juu kule UN kuhusu UHC mnamo 2019 ili kuanzisha mifumo ya kushiriki kijamii kwa ajili ya utoaji uamuzi wa afya.<sup>15</sup> Hata hivyo, kuhusishwa kwa jumuiya na vyama vya kiraia bado si toshelevu. Mitindo ya hivi majuzi katika nchi nyingi kubana nafasi ya vyama vya kiraia kunaleta uwezekano mkubwa wa kutoaminiana ambaa unatishia afya ya umma.

Kuhusisha makundi mbalimbali kotekote kwenye jumuiya kutaongeza miitikio ya sera ya kueleweka na kupunguza hali za kutokuwa na usawa wa afya ndani ya nchi na unafaa kuwa uti wa mgongo wa ufufusi. Janga limeonesha umuhimu mkubwa wa imani ya umma

Ukosefu wa kuaminiana unadhalilisha miitikio ya sera na kuongeza hali za kutokuwa na usawa, kwa kupunguza utiifu wa mwongozo wa afya ya umma, uzuiliaji wa utoaji wa chanjo, na kuvunja mioyo ya watu dhidi ya kutafuta utunzaji wa afya kwa wakati unaofaa. Kushiriki kutoka kotekote kwa jumuiya katika utoaji uamuzi ni msingi muhimu wa kufungamanisha uaminifu, kupambana na taarifa zisizofaa, na kupunguza nafasi fikiriwa kati ya mamlaka ya umma, mifumo ya afya na umma.

Kwenye janga la COVID-19, mashirika mengi ya vyama vya kiraia (CSOs) na vyama vya kitaalamu vya afya yameingilia kati ili kutoa usaidizi kwa watu wanaoishi na NCDs pale ambapo huduma za umma hazikupatikana zikiwemo utumaji wa dawa nyumbani, kusafirisha watu kwa miadi ya hospitali, na kutoa ushauri na usaidizi. Hali hii inafaa kuungwa mkono kwa rasilimali endelevu ili ziweze kushirikiana sako kwa bako na serikali katika kuunda na kutekeleza mwitikio na mipango ya ufufusi kulingana na hali yao ya uzoefu.

#### Mifano ya kuhemsha:

Chama cha kiraia cha NCD na uwakilishwaji wa wagonjwa nchini **Ufilipino**, wakiwemo Mashujaa wa Saratani Ufilipino, wamewakilishwa kwenye baraza la kitaifa la ushauri kuhusu dawa, na wamehusishwa kwenye mikutano ya dharura kwa mwitikio wa COVID-19.

Nchini **India**, Wakfu wa Blue Circle (mwanachama wa Muungano wa India yenye Afya) ulihamasisha watu waliojitelea katika kuhakikisha kwamba watu wanaoishi na kisukari wanasaidiwa; kwa mfano, kupidita kwa laini maalum za usimu ambapo watapewa ushauri au kuwa na dawa muhimu wanazohitaji kutumwa katika nyumba zao.



**Wakati mifumo ya afya inapofuzu tunanawiri; wakati inaposhindikana tunalipia kupidita kwa maisha yetu.**

**Mifumo yote ya afya inafaa kupatia kipaumbele ujumuishwaji wenye thamani wa watu walio na uzoefu wa kuishi na magonjwa ya kuambukiza na yasiyoambukiza katika sera zote za afya ya maendeleo na utekelezaji, ukiwemo mwitikio wa COVID-19 na Uwepo wa Afya Ulimwenguni."**

**Maoni Yetu, Mwanachama wa Kamati ya Ushauri Ulimwenguni kuhusu Sauti Zetu, Kenya**



## MAPENDEKEZO #3

## Fikiri upya kesi ya uwekezaji ya NCDs, ukitilia thamani katika ulinzi na usawa

Ufadhili wa kimataifa wa mwitikio wa COVID-19 ulihamasishwa ukiwa umechelewa na unatoa maelezo kidogo sana ya kuelezea bidhaa za umma ulimwenguni "ambazo zinafadhiliwa kwa kiwango kidogo sana" zinazotambuliwa na Jopo Huru la G20 kwa ajili ya Kujitayarishia na Kuitikia Janga na Jopo Huru la Kiwango cha Juu Zaidi kuhusu Ufadhili wa Mikakati Ulimwenguni wa Kujitayarishia na Kuitikia Janga.<sup>16</sup> Vilevile yayo hayo yanaweza kusemwa kuhusu NCDs zinazobakia kuwa vyanzo vikubwa zaidi vya vifo vya mapema na ulemavu kote ulimwenguni, lakini kwa sasa zinavutia chini ya 2% ya ufadhili wa afya ulimwenguni.<sup>17</sup>

Muongano wa NCD unaunga mkono mapendekezo ya majopo kuhusu uhamasishwaji ulimwenguni wa ufadhili unaohitajika dhidi ya majanga, lakini unatilia mkazo kwamba uwekezaji wa mwitikio wa janga lazima uunde silo nyingine inayolenga kuzungumzia ugonjwa kwa njia mahususi. Mtazamo wa usalama fiche unakumbwa na hatari kubwa zaidi ya kuvuruga hali ya kutokuwa na usawa na ubora. Hali ya kuficha maelezo kwa muda mrefu katika afya ya ulimwenguni, huku hufadhili na wafanyakazi wa afya wakizuiliwa kwa miitikio fulani ya ugonjwa au makundi mahususi ya idadi ya watu, vyote hivi vikikosa kutambua kwa utoshelevu yale manufaa yaliyopo ya uwekezaji katika utunzaji wa kimsingi wa afya na kinga ya NCD. Janga hili linaleta funzo kubwa kwamba watu haohao walioathiriwa na au walio katika hatari ya magonjwa maambukizi vilevile wanayo mahitaji mapana zaidi ya afya, yakiwemo NCDs na afya ya kiakili.

Wakuu wa Serikali, Wizara za Fedha na taasisi za kimataifa zinaffaa kuchunguza kesi ya uwekezaji ili kuunda NCDs kuwa kipaumbele katika upangiliaji, ukitilia maanani thamani ya afya, idadi ya watu wanaonyumbuka na kuzalisha kama kifaa muhimu na chenye maana katika gharama za afya za siku za usoni kwa NCDs na magonjwa ambukizi. Kesi hii ya uwekezaji inafaa kuongoza ugamvi wa

rasilimali za ndani, sera zinazotumika, usaidizi wa maendeleo, na mifumo thabiti ya kimataifa ambayo mahususi kama vile Kiunganishi cha Mifumo ya Afya ndani ya Kichapuzi ACT (Ufikivu wa Zana za COVID-19), ukiratibiwa na Fuko la Fedha la Ulimwenguni, Benki ya Ulimwenguni na WHO.<sup>18</sup>

Kwa mujibu wa hali tuliyopitia ya janga hili kuu la NCDs na COVID-19, serikali na wafadhili wa kimataifa wanaffaa kutoa thamani kubwa zaidi kwa kesi hii ya uwekezaji kwa ajili ya afya ya umma na sera za NCD. Fungu la sheria za WHO zilipendekezea NCD kuingilia kati ili ziweze kupatiwa nguvu na kupanuliwa, ukiakisi thamani ya ulinzi ulioboreshwa na unyumbukaji, na kupunguzwa kwa hali ya kutokuwa na usawa katika uchambuzi ule wa manufaa ya gharama. Upanuzi uweze kujumuisha mapendekezo ya sera ili kupunguza uchafuzi wa hewa, na kuboresha afya ya akili ambayo haijapitilizwa na inafaa kuzidishwa kwa ajili ya athari mbayaza janga kwa jumuia hasa afya ya aili na katika maeneo yaliyo na ubora mbovu wa hewa. Kesi ya uwekezaji ya NCD hasa kuhusiana na sera za kinga (kujumuisha ndani ya mazingatio mengine ya afya ya ulimwenguni kama vile afya ya mama na mtoto, na watu wanaoishi na au walio katika hatari ya VVU, kifua kikuu au malaria) wanaffaa pia kutilia maanani manufaa yale mapana zaidi na saidizi ya afya na kinga ya ugumu na matatizo mbalimbali, ambayo huongeza pakubwa gharama ya utunzaji wa afya na hali ya kuweza kuambukizwa na magonjwa ambukizi.<sup>19</sup>

## Mifano ya kuhemsha:

**Bhutan** anaunda mpango wa kuchukua hatua baina ya sekta mbalimbali za kitaifa kuhusiana na NCDs, huku akitambua muunganisho kati ya vifo ya COVID-19 na NCDs na akijumuisha vigezo vya mambo muhimu yanayohusika katika hatari kubwa za magonjwa yanayohusiana na moyo na kisukari.

**Wafilipino** wameendelea kuongeza mgao wa ushuru uliongezwa bidhaa za tumbaku wakati wa janga la COVID-19, huku mgao huo wa ushuru ukipang'wa mahususi kuzidisha uwezo wa UHC ili kufikia jumuia zile masikini zaidi.

**Bajeti ya India** kwa mwaka wa bajeti ambao unaanza Aprili 1 2021 inaongeza zaidi ya maradufu matumizi ya utunzai wa afya wa kitaifa na hali njema hadi trilioni 2.2 za rupi (US bilioni \$30.1). Imetengwa ili kuimariswa uwezo wa utunzaji wa Kimsingi, saidizi na husika, kupatia Kituo cha Kitaifa cha Kudhibiti Magonjwa, na kuboresha usafi na ubora wa hewa.

Tunakaribisha kujitolea kwa kuongeza

ufadhili wa ndani na usaidizi wa maendeleo katika kufikia Uwepo wa

Afya Ulimwenguni. UHC kwa kweli imekosa mwelekeo kwa sababu haifikii watu wote. Kuna pengo kati ya kujitolea na hatua, na mpaka pale ambapo lengo hili kati ya kujitolea kulikofanywa na hatua iliyofanywa litakapozibwa, ulimwengu utaendelea kuubeba mzigو wa ulemavu na vifo kutokana na NCDs."

**Maoni yetu, Mwanachama wa Kamati Shauri ya Ulimwenguni ya Sauti Zetu, Nigeria**

[M]ifumo ya afya inafaa kufikiri upya kwa

mujibu wa janga [...] na kuhudmia kwa njia bora zaidi kusudio la kujitayarishia

na kuitikia kwa mabaya na hatari za siku za usoni yanayotarajiwa (na yasiyotarajiwa), na kuzalisha jumuia zenye afya zaidi na zenye kunyumbuka zaidi. [...] Kuwa na dhana mpya ya mifumo ya afya kunamaanisha kubadilisha uwekezaji wa siku za usoni hadi kwa kazi hizi za kupatia nguvu mifumo ya afya na kuzuia kusambaratika zaidi kwa uwekezaji mwingine pinzani katika ulinzi wa afya na uimarishwaji wa afya."<sup>20</sup>

**Muungano wa Sera ya Afya na Utafiti wa Mifumo**

© Nina Robinson/Getty



#4



#### MAPENDEKEZO #4

## Kufafanua upya namna ambavyo ulinzi wa afya na kujitayarishia janga kunavyopimwa

COVID-19 imeonyeshwa kwa mara nyingine, kufuatia kwa hali iliyoonekana kwenye majanga ya SARS na MERS, kwamba watu wanaoishi na NCDs wako katika hatari kubwa zaidi na watu wanaoishi na NCDs mbalimbali ndio walio katika hatari kubwa zaidi kwenye migogoro ya afya.

Kwa mfano, uhakiki wa hatua kwa hatua na uchambuzi husika vyote vimeonyesha kwamba watu wanaoishi na unenepaji usio wa kawaida wamehusishwa na hali za mishipa ya moyo na utenda kazi wa mwili ukiwemo msongo wa mawazo na kisukari, wako katika hatari kubwa zaidi Mara saba ya kupata ugonjwa hatari, kulazwa hospitalini na hatimaye kufa kutokana na maambukizi ya virusi ikiwemo COVID-19 na mafua.<sup>21</sup> <sup>22</sup> Vilevile, watumiaji wa tumbaku wako katika hatari kubwa zaidi ya kupata NCDs mbalimbali, iklwemo saratani, ugonjwa wa moyo, na ugonjwa wa mapafu, na wamepatikana kuwa katika hatari kubwa zaidi ya matokeo hatari dhidi ya COVID-19. Watu walio na ugonjwa wa ufizi vilevile wako katika hatari kubwa zaidi ya kupata COVID-19 na wanaweza kuwa katika hatari mara tisa zaidi ya kufa, hatari mara nne zaidi ya kulazwa kwenye kitengo cha wagonjwa mahututi na mara tano zaidi ya kuwa katika hatari ya kusaidiwa kupumua.<sup>23</sup>

Hadi sasa Taratibu za Afya za Kimataifa, mnara wa Dharura za Afya za WHO, na Kiolezo cha Ulinzi wa Afya Ulimwenguni bado havijafikiria kuhusu kiwango ambacho uwepo wa NCD huwaweka idadi ya watu na uchumi kwa hatari isiyohitajika. Wakati zinalenga kupatia nguvu mifumo ya afya, serikali zimeegemea upande wa kuzingatia mtazamo wa ulinzi wa afya au ule wa UHC, lakini hivi havifai kuchukuliwa kama vibadala vya kipekee husika.<sup>24</sup> Waundaji sera walikosa fursa ya kudhibiti na kupunguza upatikanaji katika majanga kwa kuchukua hatua dhidi ya hatari maarufu, zikiwemo NCDs kwa kutoa UHC. Huku Benki ya Ulimwenguni na WHO ikitambua afya ya idadi ya watu kama rasilimali ya kiuchumi kwenye dhana ya mtaji wa binadamu, hali hii haijapata umaarufu unaohitajika katika kubadilisha mtazamo wa kisiasa.

Kama ilivyo takriban nusu ya NCDs zinaweza kuzuiliwa kuititia kwa hatua ya hatari maarufu (tumbaku, na matumizi ya pombe, uchafuzi wa hewa, kutoshughulika kimwili na matumizi ya vyakula na vinywaji visivyo na afya na vilivytengenezwa viwandani), serikali, taasisi za kimataifa na viwango vya kujitayarisha lazima zitambue jumuiya ambazo zimeathirika na athari hizi, jambo ambalo huongeza kuathirika kwao katika majanga ya siku zijazo.

Hivyo basi ni lazima kujumuisha vionyeshi vya NCD katika uchunguzi na uhakiki wa mara kwa mara kuhusu marika wa ulimwenguni dhidi ya kujitayarisha na uwezo wa kuitikia janga la kitaifa. Upana wa kazi unaendelea kupimwa kuhusu namna ya kuhusisha NCDs kwenye mipasho ya Kiolezo cha Ulinzi wa Afya Ulimwenguni na unafaa kufungamanishwa kwenye ukadiriaji wa kimataifa kuhusu kujitayarishia kunakozungumziwa kwa muktadha wa janga linalowezekana. Kwa mfano, data iliyoripotiwa kwa WHO kwa mujibu wa mpangilio wa ufuutiliaji ulimwenguni wa NCD unaweza kutumika kwa kusudio hili. Pale ambapo hali hiyo haijatokea, uwepo wa NCD na data inayosababisha hatari husika inafaa kujumuishwa kaitka mifumo ya usimamizi wa taarifa ya afya ili kutoa uamuzi kuhusu mifumo ya afya ambayo inapatia nguvu na kinga sera za NCD.

### Mifano ya kuhemsha:

Kwa kutambua muunganisho kati ya uwepo wa unenepaji wa kupindukia na idadi ya watu walio katika hatari ya COVID-19, hatua mpya ya sera kuhusu unenepaji wa kupindukia imetangazwa kule **Uingereza**. Kule Uingereza, kumepatikana kwamba zaidi ya theluthi moja ya wagonjwa waliolazwa hospitalini kutokana na COVID-19 wamekosa shughuli za kimwili na kuwa na uzito wa mwili wa kupindukia.<sup>25</sup>

#5



## MAPENDEKEZO #5

## Angazia upya migogoro ya maslahi na kutokuwa kwa usawa wa mamlaka

Janga limezidisha utambulisho wa kutokuwa na usawa kwa mamlaka na kutilia maanani utajiri ambaa unaendelea kushawishi kwa njia isiyofaa utoaji wa uamuzi. Kuweka maslahi ya kiuchumi ya muda mfupi mbele ya afya ya umma kumesababisha kupotezwa kwa maisha na riziki.

Ufikivu usiokuwa na usawa wa chanjo za COVID-19, kwenye nchi na vilevile jumuiya, kunaonyesha kwamba mifumo thabiti ya utawala wa kimataifa inahitajika kwa miitikio bora zaidi kwa janga. Aidha, uhariibifu wa kimazingira na uchafuzi vyote vinaendelea bila kusitishwa, hali ambayo inaweka ulimwengu katika hatari zaidi ya tishio za ulinzi wa afya, kusambaratika kwa mseto wa mazingira, kuenezwa kwa magonjwa yanayoambukizwa kati ya wanyama na binadamu na upinzani wa viini mbalimbali. Kila kimojawapo cha hivi kinaweza kusababisha migogoro ya kibinadamu na kiuchumi kwa kiwango kisichotarajiwa. Maendeleo ya mkataba wa janga yanatoa fursa kwa utawala ulioboreshwala ili kuangazia tishio za afya na kuhamasisha rasilimali za kitaifa na kimataifa kwa manufaa ya umma wa ulimwenguni. Ulimwengu haufai kurudi kwa hali ya kawaida, bali kujipanga upya huku afya ikipewa kipao mbele.

Kunayo maswali mapana zaidi ya kimuundo ya kuangazia kuhusiana na utawala na afya ya kimaeneo. Uchunguzi wa kesi mbalimbali kutoka mabara yote umeonyesha kwamba viwanda vinyavodhuru afya - vikiwemo viwanda vya kisasa vya utengenezaji wa chakula na vinywaji, pombe, tumbaku, na vichafuzi - vyote vimetumia vibaya janga hili na kupata ushawishi usiokuwa na afya dhidi ya watumiaji n watoaji uamuzi.<sup>26</sup> Janga linaonyesha udharura wa kuangazia upya hali hizi za kutokuwa na usawa wa mamlaka na fursa ya mazungumzo na umma kuhusu kulinda maslahi yao na kuitikia kwa wasiwasi wa afya yao kwa njia bora zaidi.

Ushawishi wa kisia wa viwanda na makampuni ambayo mienendo na bidhaa zake ni haribifu kwa

afya lazima vifutiliwe kwa umakini na kudhibitiwa vilivyo. Serikali lazima ziwezeshwe kupertia kwa utawala bora zaidi ili kugeuza sheria ile ya 'mashindano ya kueleke chini' na kuweka afya ya umma kwanza, ili kuvuka mapungufu ya ushuru baina ya mipaka, ada dhidi y ushuru kwa bidhaa zinazodhuru afya na kuondoa usaidizi unaodhuru afya, ukiwemo ule wa kuunga mkono uzalishaji na umarishwaji wa tumbaku, pombe, vyakula na vinywaji vilivytengenezwa kwa viwanda vya kisasa, na mafuta taa. Mapato na akiba zinazotokana na haya yote yanafaa kutumika kuimarishe kwa njia bora zaidi - kwa ulinzi wa afya na afya - kuimarishe bidhaa na huduma za umma.

### Mifano ya kuhemsha:

#### Janga limezidisha suluhu kwenye uwanja wa afya ya kileo:

Imependekezwa kwa muktadha wa janga **Muungano wa Ulaya** utachukua furushi la kisheria katika kutekeleza vilengwa vya hali ya hewa na kuwa bara la kwanza la kutokuwa na uchafuzi wa hewa wa Carbon, ikisema "Mwongo huu unatupa muda wa kufaulu au kufeli kaitka utekelezaji wa kujitolea kwetu kwa mujibu wa Mkataba wa Paris, kwa maslahi ya afya, hali njema, na ufanisi kwa wote."<sup>27</sup> Taasisi za Muungano wa Ulaya zinaendeshwa kwa Sajili ya Uwazi ili kufuatilia na kuchapisha shughuli za uhamasishwaji.<sup>28</sup>

Kwenye **Visiwa vya Pacific**, jitihada zinaendelea kuzidishwa ili kurudisha mazoea ya kitamaduni ya ulaji na kupunguza ulaji wa bidhaa zisizo na afya na zilizotewa kutoka kwingineko. Serikali nchini Fiji kwa mfano ilianza kusambaza mbegu kwa wakazi kwenye kipindi cha kuwafungia nchi ili kuhakikisha ugavi salama wa chakula chenye afya katika nchi ambapo 16% pekee ya idadi ya watu wako na umri wa zaidi ya 55 kutokana na vifo vya mapema ambavyo vimesababishwa kimsingi na NCDs.

Nchini **Namibia, Zambia, Afrika Kusini na Sierra Leone**, watu wanaoishi katika nyumba za vibanda mijini wanapokea usaidizi wa ulimaji wa ndani na miradi mingineyo kama hiyo ili kuimarishe ulinzi wa chakula chenye lishe bora na riziki thabiti zaidi.<sup>29</sup>

Mijini **Bogota, Paris na London**, madiwani wanawekeza kwa nia ya kuongeza mtandao wa safu salama za kuendeshea baiskeli ili kuwafanya watu kushughulika na kuwapunguza wao kujaa katika uchukuzi wa umma. Kama athari yenye afya, hali hii inaangazia mambo mawili ya NCD kati ya matano makuu yanayosababisha hatari - uchafuzi wa hewa na ukosefu wa mazoezi.



## MNARA WA 2

### Kinga: Zingatia idadi ya watu kama njia ya kujitayarishia

Idadi ya watu wenyewe afya ndiyo msingi wa ulinzi, unyumbukaji, kujitayarishia tishio za afya na maendeleo ya kiuchumi. Hivyo basi ni muhimu kuwekeza kwenye uimarishaji wa afya, kinga ya NCD, uchunguzi na ugunduzi kama sehemu ya mwitikio wa janga, ufufuzi na kujitayarishia siku za usoni. Umakinifu ulioongezeka kwa makundi yaliyo katika hatari na kuzingatia lile pengo la ugunduzi ni kipengele muhimu kinachofaa kuangaziwa, kwani ugunduzi wa mapema unaruhusu ugumu zaidi na changamoto nyinginezo kuweza kuzuiliwa.<sup>30</sup> Kwa mfano, nusu ya watu wazima wanaoishi na kisukari hawajagunduliwa bado na hata ndani ya nchi zenye mapato ya juu pekee mmoja kati ya watu watano anaishi na msongo wa mawazo na amedhibitiwa na matibabu. Watu wanaoishi na msongo wa mawazo, kisukari, na/au ugonjwa hatari wa figo walipitia vizuizi vya wao kufikia utunzaji wa afya na kuzoroteka kwa dalili zao wakati wa janga, vyote ambavyo vilikuwa pamoja na kupoteza pakubwa mapato na ajira, na tofauti zinazoendelea kuwepo za afya na mambo ya kijamii na kiuchumi.<sup>31,32</sup>

66

**Wale wanaoishi na NCDs ndiyo hasa walioathirika. Kiwango kamilifu cha haya kinaweza kutojulikana, kwa sababu ya kesi nyingi ya NCDs ambazo hazingunduliwi. Kinga na udhibiti wa NCDs hivyo basi una wajibu mkuu katika mwitikio wa COVID-19. Kama mwitikio wa COVID-19 hautalinganiswha ili kujumuisha kinga na usimamizi wa hatari za NCD, huenda tutashinda kuwafaa watu wengi kwa wakati ambao kinga yao imedhoofika.”<sup>33</sup>**

Dkt Hans Henri P. Kluge, Mkurugenzi wa Kimaeneo wa WHO, Ulaya.





## MAPENDEKEZO #6

## Kiini cha kinga

Janga linaleta jambo la lazima la kuweka upya na kujipanga upya katika sera ili kuimarisha kwa njia bora zaidi na kwa umaizi zaidi. COVID-19 na NCDs vyote vinawakilisha hasara kuu kwa mujibu wa binadamu, na vilevile rasilimali yenye thamani zaidi itokanayo na nchi husika – werevu, ubunifu, na uzalishaji wa watu wao.

Viongozi lazima wabadilishe mazingatio yao ili kuwa na idadi ya watu wenye afya zaidi, pamoja na rasilimali na mtaji wa kisiasa wa kuweza kuwekeza katika kinga ya magonjwa mbalimbali. Sera za ufufuzi lazima zitimize hatua ya mabadiliko kwa jumuiya na mazingira ambayo yanaimarisha afya na hali njema. Kile ambacho kinahitajika zaidi kiko nje ya maeneo ya wizara za afya, na kinahusisha uchumi, biashara, mazingira, nishati uchukuzi, maendelo ya mijini, kilimo, na mifumo ya chakula kwa hivyo uongozi lazima uanzie kwenye uongozi wa juu wa serikali husika. Hali hii inajumuisha utekelezaji wa sheria na taratibu ambaa umethibitishwa kuwa wenye gharama nafuu katika kuzuia mseto wa NCDs - ithibati iliyopo itokanayo na WHO inayozungumzia mapendekezo ya uingiliaji kati.<sup>34</sup>

Kuendeleza na kuboresha afya ya idadi ya watu kutasaidia dhidi ya tishio za afya za siku za usoni na kuzuia gharama za migogoro ya afya za siku za usoni. Mambo makuu mbalimbali yanayohatarisha NCDs huongeza hatari ya magonjwa makali na vifo kutokana na COVID-19, yakiwemo matumizi ya tumbaku, ulaji usiokuwa na afya na kutofanya mazoezi ya kutosha (uzito wa kupindukia na unenepaji usiofaa), na kuwepo ndani ya uchafuzi wa hewa. NCDs zimefichua nchi mbalimbali dhidi ya hatari isiyohitajika kwenye mikurupuko ya ugonjwa, lakini NCDs nydingi zinaweza kuzuiliwa kikamilifu. Tumbaku, uchafuzi wa hewa na NCDs zinazohusiana na ulaji kwa sasa hivi zinakadiriwa kuwa ndizo chanzo cha takriban vifo vya mapema vya watu milioni nane kote ulimwenguni kila mwaka, huku vifo vingine zaidi vya watu milion tatu vikirekodiwa kuhusiana na matumizi ya pombe. Wingu wa gharama hii ya binadamu na kiuchumi, ukiwemo ugumu wa gharama na bidhaa husika kuweza kubadilishwa kuititia kwa sera ambazo zimejaribiwa na kupimwa.<sup>35</sup>



© Frame Convention Alliance

Miongoni mwa mataifa mbalimbli, janga tayari limezidisha mabadiliko muhimu ya sera; mfano, kuanzhishwa kwa lebo za onyo za kuwekwa mbele juu ya mfuko wa kubebwa kwa ajili ya vyakula visivyo na afya, kusaidia uchukuzi amilifu ndani ya miji, kutoza ushuru wa kiwango cha juu zaidi kwa tumbaku na vinywaji vilivyoongenzwa utamu wa sukari, kupigwa marufuku kwa mafuta yaliyotengenezwa, vizuizi vyakula kwa pombe, kupigwa marufuku kwa utangazaji na uuzwaji wa vitafunio shulenii, na mambo ya kufuatwa ili kupunguza uchafuzi wa hewa. Baadhi ya mashirika ya kimataifa yanaunda mitazamo mipya ya Afya Moja na Afya ya Kileo zikiwemo sera za kinga ya NCD; kwa mfano, Manifesto ya WHO juu ya Ufufuzi wenye Afya<sup>36</sup> na Mpango wa Muungano wa Ulaya wa Kupambana na Saratani.<sup>37</sup>

### Mifano ya kuhemsha:

Kutambua idadi isiyoleweka ya kesi za COVID-19 miongoni mwa watoto na watu wazima walio na uzito wa kupindukia, **Majimbo ya Meksiko ya Oaxaca na Tabasco** yalipiga marufuku uuzaji wa vitafunio na vinywaji vyenye sukari kwa watoto walio chini ya umri wa miaka 18 na walio pekee yao mnamo 2020, huku majimbo mengi zaidi yakipangilia kufanya hivyo. Sheria ya **Meksiko** ya nchini kote inayotoa onyo kwa lebo zinazowekwa kwenye mifuko ya kubebwa chakula, iliyokielezeo cha sheria mojawapo ambayo tayari ili kuwa imetekelezwa kule Chile, zilianza kutekelezwa mnamo Oktoba 2020 zikhijaji ishara nyeusi za kukomesha kwenye mifuko ya vyakula vyenye sukari iliyoongezwa, mafuta (yaliyokolezwa na mafuta yale mengine) kalori na sodiamu iliyoongezwa. Hakuna chochote kilicho na ishara nyeusi za kukomesha kuuzwa kinaweza kuuzwa au kupigwa debe shulenii, na hivyo kuwalinda zaidi watoto.

**Cambodia, Eswatini, Georgia, Jordan, Myanmar, Serbia na Sri Lanka** wameweza hususan kutaja umuhimu na ufaavu wa mbinu za kudhibiti tumbaku na/au utekelezaji wa Mpangilio wa Makubaliano kuhusu Udhibiti wa Tumbaku katika mwitikio wao wa kitaifa na mipango ya ufufuzi kuhusu COVID-19.

#7



## MAPENDEKEZO #7

## Kabiliana na hali zisizokuwa na usawa kupitia kwa ulinzi wa kijamii wenyewe ubora zaidi

Uongozi unahitajika ili kugeuza mabadiliko ya kutokuwa na usawa. Pengo la afya linalozidi kuwa pana zaidi limeweza kusababishwa na athari za kutokuwa na usawa dhidi ya COVID-19 kwa makundi na jumuiya tofauti za kijamii na kiuchumi.<sup>38</sup> Utofauti katika kutarajiwa kwa maisha kwa makundi yaliyotengwa na kudhulimiwa unaonyesha mtagusano usio sawa wa hatari mbalimbali za NCD na vizuizi vya kimuundo kwa afya ambavyo vimeendesha janga kuu la COVID-19 na NCDs.

COVID-19 inaendelea kuzidisha hali za kutokuwa na usawa ambazo ziliwaweka baadhi ya watu katika hatari kubwa zaidi kwa kila mgogoro, hajjalishi kama ilikuwa janga, mgogoro, au athari za mabadiliko ya hali ya hewa. Miongo minne ya kupitia hali ya kupambana na VVU/UKIMWI imeonyesha njia: Hatua ya sera, usaidizi wa jumuiya na ushirikiano wa mataifa katika kufunga mapengo ya afya na kutoacha mtu ye yeyote nyuma ndiyo njia ya pekee ya kukomesha majanga.

Serikali na jumuiya ya afya ya ulimwenguni na maendeleo lazima zitambue hali za kutokuwa na usawa ambazo zinaamua pakubwa ni nani anayefikia mazingira ya afya, na nani anafikia huduma za afya na utunzaji ambaio unatimiza mahitaji yao na ni nani ananyimwa na kuachwa nyuma. Vizuizi hivi lazima viondolewe kupitia kwa sheria, sera, na programu za ulinzi wa kijamii zilizoundwa ili kulinda kila mmoja, kuleta kila mmoja pamoja kwa ajili ya ufufuzi. Vizuizi hivi vinajumuisha umaskini, ubaguzi wa rangi, ubaguzi, aina zote za utapia mlo (ukiwemo uzito wa mwili wa kupindukia na unenepajji usio wa kawaida<sup>39,40</sup>), ajira isiyo na uhakika, elimu na upangaji mbovu, na mazingira yasiyokuwa salama au machafu, pamoja na vizuizi vya kufikia utunzaji wa afya.

**Mfano wa kuhemsha:**

Ille **Serikali ya Wales** imezingatia kiini cha usawa wa mipango yao ya ufufuzi, huku ikitoa uanzilishi wa Ripoti ya Hali ya Usawa wa Afya ya Wales (WHSRI) yenye kichwa Kuweka usawa wa afya katika kitovu cha mwitikio endelevu na ufufuzi wa COVID-19: Kujenga maisha yaliyoimarika kwa wote walio Wales.<sup>41</sup>

**Hatuwezi kuharibu muda katika kuunda jumuiya bila ya unyonge uliozua mwitikio wetu wa COVID-19."**

**Profesa Sandro Galea, Mkuu wa Kitengo cha Chuo Kikuu cha Boston Shule ya Afya ya Umma.**



© Russel Watkins

## MNARA WA 3


### **Mifumo ya afya:** Mizuri zaidi na inayofaa kwa ajili ya siku za usoni

Uchambuzi wa majanga ya awali ulihitimisha kwamba mifumo ya afya ya kitaifa yenye ubora ndiyo mstari wa kwanza wa ulinzi. Unyumbukaji wa mfumo wa afya unafisiliwa kama "uwezo wa wahuksika wa afya, taasisi, na idadi ya watu katika kujitayarisha na kuitikia kikamilifu kwa migogoro; kuendeleza kazi kuu wakati mgogoro unapoibuka; na kufanya kueleweka vizuri zaidi kupitia kwa mafunzo husika kwenye kipindi hicho cha mgogoro kupangilia upya kama hali zitahitaji kufanya hivyo".<sup>42</sup> Ufasili huu unatumika katika muktadha wa mikurupuko ya magonjwa na majanga isiyotarajiwa, lakini vilevile mpito wa kiepidimiolojia kwa NCDs kuwa vyanzo vikuu vya vifo na magonjwa kwenye maeneo yote ya ulmwenguni. Ukatizaji mkuu wa huduma za kimsingi za NCD uliosababishwa na COVID-19 kutoka kote ulmwenguni umeangazia kwamba mafunzo kutoka kwenye majanga ya awali hayakuwa yamefaa jumuiya ya kimataifa wala kuonekana katika uwekezaji wa serikali za kitaifa ndani ya mifumo ya afya.



## Mchoro wa 2: Nchi zinazoripoti ukatizwaji wa huduma za NCD.

